# Ofisi ya Taifa ya Takwimu

S. L. P 796 Simu: 255- (022) 2122722/3/4 Nukushi:+225 (022)2130852
Dar es Salaam,-TANZANIA Barua pepe: dg@nbs.go.tz


*Unapojibu tafadhali taja:*
Kumb Na: NBS/S.40/21/484

**YALIYOJITOKEZA**

Tarehe: 08 Januari, 2014

## FAHIRISI ZA BEI ZA TAIFA MWEZI DESEMBA, 2013

## Utangulizi

### Maana ya Fahirisi za Bei za Taifa

Fahirisi za bei za Taifa ni kipimo kinachotumika kupima mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma mbalimbali zinazotumiwa na jamii. Bei za bidhaa na huduma zipatazo 224 hukusanywa kila mwezi kwa kila mkoa nchini.

### Mizania mpya za bidhaa na huduma za jamii na kizio cha bei

Mizania ya Fahirisi za bei za Taifa zimetokana na matumizi ya kaya binafsi kutoka mikoa 21 ya Tanzania Bara. Mizania inajumuisha matumizi ya kaya zote binafsi kutoka mijini na vijijini. Kizio cha Fahirisi za Bei za Taifa kimebadilishwa kutoka Februari 2001=100 hadi Septemba 2010=100.

### Makundi ya bidhaa na huduma za jamii

Marejeo ya Fahirisi za Bei za Taifa yamefanyika kwa kufuata makundi yaliyokubalika Kimataifa yanayoitwa mchanganuo wa matumizi binafsi "Classification of Individual Consumption by Purpose (COICOP)". Fahirisi mpya za Bei inajumuisha makundi 12 ya mfumo wa COICOP pamoja na fahirisi za bei kwa makundi maalumu. Makundi hayo maalumu ni; 1) Vyakula na vinywaji baridi-vikijumuisha vyakula vinavyoliwa majumbani na mahotelini; 2) Nishati na Mafuta - kundi hili linajumuisha umeme na aina nyingine za nishati zinazotumika majumbani pamoja na petroli na dizeli; 3) Fahirisi za bidhaa na huduma zote za jamii isipokuwa vyakula na vinywaji baridi; 4) Fahirisi za huduma zote za jamii isipokuwa vyakula, vinywaji baridi, nishati na mafuta.

### Namna ya kukokotoa Fahirisi za Bei za Taifa

Maboresho yamefanyika kwenye ukokotoaji wa Fahirisi mpya za Bei za Taifa, ikiwa ni pamoja na kutumia wastani wa jiometria "geometric means" kwenye kukokotoa Fahirisi za Bei katika ngazi za mwanzo badala ya wastani wa kawaida "arithmetic mean", matumizi ya mfumo ulioboreshwa wa ukokotoaji pamoja na mfumo mzima wa kukusanya na kuchambua bei. Kanuni ya "modified Laspeyres index" inaendelea kutumika kukokotoa Fahirisi za Bei za Taifa katika ngazi ya makundi makubwa.

## MFUMUKO WA BEI KWA KIPIMO CHA MWAKA UMEPUNGUA HADI ASILIMIA 5.6

### Jedwali Namba 1: Badiliko la Fahirisi za Bei za Taifa kwa Mwezi Desemba, 2013 (Septemba, 2010 = 100)

| Na. | KUNDI (MAIN GROUP) | Mizania (Weight) | Des-12 | Nov-13 | Des -13 | Badiliko la mwezi mmoja | Badiliko la miezi 12 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Vyakula na vinywaji baridi | 47.8 | 148.23 | 154.05 | 157.15 | 2.0 | 6.0 |
| 2 | Vinywaji vyenye kilevi na bidhaa za tumbaku | 3.3 | 130.89 | 141.02 | 141.12 | 0.1 | 7.8 |
| 3 | Mavazi ya nguo na viatu | 6.7 | 126.02 | 130.63 | 130.89 | 0.2 | 3.9 |
| 4 | Nishati, Maji na Makazi | 9.2 | 143.59 | 155.41 | 158.30 | 1.9 | 10.2 |
| 5 | Samani, vifaa vya nyumbani na ukarabati wa nyumba | 6.7 | 125.65 | 128.09 | 128.56 | 0.4 | 2.3 |
| 6 | Gharama za Afya | 0.9 | 106.87 | 108.50 | 108.49 | 0.0 | 1.5 |
| 7 | Usafirishaji | 9.5 | 115.97 | 125.17 | 125.43 | 0.2 | 8.2 |
| 8 | Mawasiliano | 2.1 | 96.28 | 96.61 | 96.73 | 0.1 | 0.5 |
| 9 | Utamaduni na Burudani | 1.3 | 111.78 | 112.87 | 112.85 | 0.0 | 1.0 |
| 10 | Elimu | 1.7 | 110.75 | 113.38 | 113.40 | 0.0 | 2.4 |
| 11 | Hoteli na Migahawa | 6.4 | 131.90 | 134.69 | 134.74 | 0.0 | 2.2 |
| 12 | Bidhaa na huduma nyinginezo | 4.5 | 118.48 | 122.91 | 123.22 | 0.3 | 4.0 |
| **JUMLA – FAHIRISI BIDHAA ZOTE** | | **100** | **136.48** | **142.23** | **144.07** | **1.3** | **5.6** |
| **Makundi Mengine Teule** | | | | | | | |
| 1 | Vyakula—vikijumuisha vyakula vilivyoliwa majumbani na mahotelini | 51.0 | 146.44 | 153.17 | 156.08 | 1.9 | 6.6 |
| 2 | Nishati na Mafuta—kundi hili linajumuisha umeme na aina nyingine za nishati zinazotumika majumbani pamoja na petroli na dizeli | 5.7 | 158.12 | 173.69 | 178.39 | 2.7 | 12.8 |
| 3 | Fahirisi za bidhaa na huduma zote za jamii isipokuwa vyakula na vinywaji baridi | 49.0 | 124.69 | 130.81 | 131.55 | 0.6 | 5.5 |
| 4 | Fahirisi na huduma zote za jamii Isipokuwa vyakula, nishati na mafuta | 43.3 | 119.66 | 124.90 | 125.09 | 0.2 | 4.5 |

Mfumuko wa Bei wa Taifa kwa kipimo cha mwaka unapima kiwango cha badiliko la kasi ya bei za bidhaa na huduma zote zinazotumiwa na kaya binafsi. Jedwali namba 1 hapo juu linaonyesha kwamba, Mfumuko wa Bei wa Taifa kwa mwezi Desemba, 2013 umepungua hadi asilimia 5.6 kutoka asilimia 6.2 mwezi Novemba, 2013. Kupungua kwa Mfumuko wa Bei wa mwezi Desemba, 2013 kunamaanisha kuwa, kasi ya upandaji wa bei za bidhaa na huduma kwa mwezi Desemba, 2013 imepungua ikilinganishwa na kasi ya kupanda kwa bei kwa mwezi Novemba, 2013. Aidha, Fahirisi za Bei zimeongezeka hadi 144.07 kwa mwezi wa Desemba, 2013 kutoka 136.48 mwezi Desemba, 2012. Mfumuko wa Bei wa Vyakula na Vinywaji Baridi umepungua hadi asilimia 6.0 mwezi Desemba, 2013 kutoka asilimia 7.2 ilivyokuwa mwezi Novemba, 2013.

### Mfumuko wa Bei kwa Bidhaa za Vyakula na Bidhaa Zisizo za Vyakula


Badiliko la Fahirisi za Bei za bidhaa za vyakula nyumbani na migahawani limepungua hadi asilimia 6.6 mwezi Desemba, 2013 ikilinganishwa na asilimia 7.6 mwezi Novemba, 2013. Badiliko la Fahirisi za Bei kwa bidhaa zisizo za vyakula limepungua hadi asilimia 5.5 kwa mwezi Desemba, 2013 kutoka asilimia 5.7 mwezi Novemba, 2013.

**Mfumuko wa Bei wa Bidhaa na Huduma Zote Isipokuwa Bidhaa za Vyakula na Nishati**

Aina hii ya Fahirisi haijumuishi vyakula vilivyoliwa nyumbani na migahawani, vinywaji baridi, petroli, dizeli, gesi ya kupikia, mafuta ya taa, mkaa na umeme. Vyakula na nishati vina sifa ya kuwa na bei ambazo hubadilika mara kwa mara hivyo vikiondolewa kwenye Fahirisi ya bidhaa na huduma zote hubakia Fahirisi ambayo ina mwelekeo imara kwa Watunga Sera.

Mfumuko wa Bei ambao haujumuishi vyakula na nishati kwa mwezi wa Desemba, 2013 umepungua zaidi hadi asilimia 4.5 ikilinganishwa na asilimia 5.3 mwezi Novemba, 2013.

**Kielelezo Namba 1: Mwenendo wa Fahirisi za Bei za Taifa na Mfumuko wa Bei Kutoka Desemba, 2012 Hadi Desemba, 2013. (Septemba, 2010 = 100)**




Kielelezo Namba 1 hapo juu kinaonyesha kuwa, katika kipindi kati ya mwezi Desemba, 2012 hadi Desemba, 2013, Fahirisi za Bei zimeonyesha mienendo tofauti. Kumekuwa na mwenendo wa kuongezeka kwa bei za bidhaa na huduma mbalimbali kutoka mwezi Desemba 2012 hadi Aprili, 2013 na mwenendo imara wa Fahirisi za Bei kutoka mwezi Mei, 2013 hadi Septemba, 2013. Hata hivyo, Fahirisi za Bei zimekuwa na mwenendo wa kuongezeka kutoka mwezi Oktoba, 2013 hadi Desemba, 2013. Mfumuko wa Bei umekuwa na mwenendo wa kushuka kutoka asilimia 12.1 mwezi Desemba, 2012 hadi kufikia asilimia 5.6 mwezi Desemba, 2013.

## MFUMUKO WA BEI KWA KIPIMO CHA MWEZI UMEONGEZEKA KWA ASILIMIA 1.3

Mfumuko wa Bei wa mwezi Desemba, 2013 umeongezeka kwa asilimia 1.3 ikilinganishwa na ongezeko la asilimia 0.6 kama ilivyokuwa mwezi Novemba, 2013. Fahirisi za Bei zimeongezeka hadi 144.07 mwezi Desemba, 2013 kutoka 142.23 mwezi Novemba, 2013. Ongezeko la Fahirisi za Bei limechangiwa na kuongezeka kwa bei za bidhaa za vyakula na bidhaa zisizo za vyakula. Baadhi ya bidhaa za vyakula zilizochangia kuongezeka kwa fahirisi ni; mchele kwa asilimia 0.2, vitafunwa kwa asilimia 2.4, mahindi kwa asilimia 1.4, unga wa mahindi kwa asilimia 1.6, unga wa muhogo kwa asilimia 3.0, kuku wa kienyeji kwa asilimia 1.5, dagaa kwa asilimia 2.1, nazi kwa asilimia 11.5,

mbogamboga kwa asilimia 5.8, nyanya kwa asilimia 8.3, njegere kwa asilimia 12.6, maharage kwa asilimia 3.7, mihogo kwa asilimia 5.1 na viazi vitamu kwa asilimia 7.2. Baadhi ya bidhaa zisizo za chakula zilizochangia kuongezeka kwa fahirisi ni; vitambaa vya suruali kwa asilimia 1.2, blauzi kwa asilimia 1.2, huduma za kufua nguo kwa asilimia 3.6, gesi kwa asilimia 3.4, mafuta ya taa kwa asilimia 2.1, mkaa kwa asilimia 4.0, mazulia na vifaa vingine vya kufunikia sakafu kwa asilimia 1.7, vyerehani kwa asilimia 1.3, dizeli kwa asilimia 1.3, petroli kwa asilimia 0.2 na huduma za usafi wa nywele pamoja na usafi binafsi kwa asilimia 1.2.


## Thamani ya Shilingi ya Tanzania Mwezi Desemba, 2013 Ikilinganishwa na Mwezi Septemba, 2010

**Tafsiri**: Thamani ya Shilingi ya Tanzania inatafsiriwa kuwa ni badiliko la Uwezo wa Shilingi ya Tanzania katika kununua bidhaa na huduma zilezile za mlaji ambazo Shilingi ya Tanzania ingeweza kununua katika vipindi tofauti. Ikiwa wastani wa Fahirisi za Bei za Taifa unaongezeka, Uwezo wa Shilingi ya Tanzania katika kununua bidhaa na huduma hupungua.

Uwezo wa Shilingi 100 ya Tanzania katika kununua bidhaa na huduma umepungua hadi Shilingi 69 na senti 41 mwezi Desemba, 2013 kutoka mwezi Septemba, 2010.

## MIENENDO YA BEI


### Kielelezo Namba 2: Mienendo ya Bei kwa Makundi Mbalimbali ya Fahirisi za Bei Kutoka Desemba, 2012 Hadi Desemba, 2013. (Septemba, 2010 = 100)




Kielelezo Namba 2 hapo juu kinaonyesha mienendo ya bei kwa makundi mbalimbali ya Fahirisi za Bei kuanzia mwezi Desemba, 2012 hadi mwezi Desemba, 2013. Kwa wastani, Fahirisi za nishati na mafuta na Fahirisi za vyakula na vinywaji baridi zimekuwa na mwenendo wa juu kwa kipindi chote zikilinganishwa na fahirisi nyingine. Kundi la nishati na mafuta limeonyesha pia kuwa na mwenendo wa fahirisi usio imara ikilinganishwa na makundi mengine kwa kipindi husika. Fahirisi za bidhaa zisizo za chakula na fahirisi za bidhaa zisizo jumuisha chakula pamoja na nishati zimeonesha mwenendo wa bei ulio imara.

## MIENENDO YA BEI NA MFUMUKO WA BEI KUTOKA JANUARI HADI DESEMBA, 2013

**Kielelezo Namba 3: Mienendo ya Bei na Mfumuko wa Bei kutoka Januari hadi Desemba, 2013 (Septemba, 2010 = 100)**




Kielelezo namba 3 hapo juu kinaonyesha mwenendo wa Fahirisi za Bei za Taifa na Mfumuko wa Bei kutoka mwezi Januari hadi Desemba, 2013. Fahirisi za Bei za bidhaa na huduma mbalimbali zimekuwa na mwenendo wa kupanda kwa kipindi chote cha robo ya kwanza ya mwaka kutoka 138.26 mwezi Januari, 2013 hadi 141.59 mwezi Aprili, 2013. Kuanzia mwezi Mei hadi Agosti, 2013 kulikuwa na mwenendo wa bei ulio imara na ulianza tena kuongezeka kuanzia mwezi Septemba hadi Desemba, 2013. Kwa wastani, Fahirisi za Bei za Taifa ziliongezeka hadi 140.83 mwaka 2013 kutoka 130.56 mwaka 2012. Bei za bidhaa na huduma zilionyesha kuongezeka zaidi mwezi Desemba, 2013 zikilinganishwa na miezi mingine. Aidha, mwezi Januari, 2013 kulikuwa na ongezeko dogo zaidi ikilinganishwa na miezi mingine. Kwa upande mwingine, Mfumuko wa Bei wa Taifa ulionyesha mwelekeo wa kushuka kutoka asilimia 10.9 mwezi Januari, 2013 hadi asilimia 5.6 mwezi Desemba, 2013.

Kwa wastani, Mfumuko wa Bei wa Taifa (kutoka Januari hadi Desemba, 2013) umepungua hadi kufikia asilimia 7.9 kutoka asilimia 16.0 iliyofikiwa mwaka 2012. Kupungua kwa wastani wa Mfumuko wa Bei wa Taifa mwaka 2013 kumechangiwa hasa na kupungua kwa kasi ya kupanda kwa bei za bidhaa za vyakula hasa mchele na aina nyingine za nafaka. Wastani wa Mfumuko wa Bei wa Bidhaa za vyakula kwa mwaka 2013 umepungua kwa kiwango kikubwa hadi kufikia asilimia 8.6 kutoka asilimia 20.2 mwaka 2012. Aidha, Wastani wa Mfumuko wa Bei wa bidhaa zisizo za vyakula nao umepungua hadi asilimia 7.5 mwaka 2013 kutoka asilimia 10.7 mwaka 2012 na wastani wa Mfumuko wa Bei ambao haujumuishi Vyakula na Nishati umepungua hadi asilimia 6.2 mwaka 2013 kutoka asilimia 8.8 kwa mwaka 2012.


**Mawasiliano: Mkurugenzi Mkuu,**
**Ofisi ya Taifa ya Takwimu**